Government of **Western Australia**
**Mental Health Commission**

wako wa magonjwa ya akili anaweza kusifa ECT kwako.

Kuna mipaka kwa hali gani ECT inaweza kutolewa. Hiyo ni:

- ECT haiwezi kutolewa kwa yeyote chini ya umri wa miaka 14.
- ECT inaweza kutolewa kwa mgonjwa mtoto wa hiari (miaka 14-17) pamoja na ruhusa yake, au kama hawezi kutoa ruhusa iliyojulishwa, pamoja na ruhusa ya mzazi au mlezi wako. Kibali cha Baraza ya Afya ya Akili kinahitajika pia.
- ECT inaweza kutolewa kwa wagonjwa wa hiari ambao ni watu wazima (miaka 18 na zaidi) pamoja na ruhusa yake, au kama hawezi kutoa ruhusa iliyojulishwa, pamoja na ruhusa ya mtu anayeruhusiwa kuamua maamuzi kwa ajili ya mgonjwa, kama mlezi.
- ECT inaweza kutolewa tu kwa wagonjwa asiyekusudiwa na kibali cha Baraza ya Afya ya Akili.

Wakati kibali cha Baraza ya Afya ya Akili ya ECT kinahitajika, mtaalum wako wa magonjwa ya akili ataomba kwa maandishi kwa Baraza na Baraza itakagua kesi yako.

Kama wewe ni mgonjwa asiyekusudiwa mtu mzima na ECT inahitajika kuokoa maisha yako au kukuzuia kusababisha madhara makali ya kimwili kwa wewe mwenyewe au mtu mwengine, ndipo kibali cha Baraza haihitajika kwa ECT. Lakini, katika kesi hii Mtaalum Mkuu wa magonjwa ya akili akubali ECT.

## Maelezo zaidi

Maelezo katika brosha hii inahusisha masheria ambayo yamo Sheria ya Afya ya Akili 2014. Maelezo kuhusu Sheria hii imefupishwa katika seti ya brosha zifuatazo:

- Kupendekezwa kwenda kwa mtaalum wa magonjwa ya akili kwa uchunguzi
- Maagizo ya matibabu kwa mgonjwa aliyelazwa hospitalini
- Maagizo ya matibabu ya jamii
- Maelezo kwa wagonjwa wa hiari
- Kupokea matibabu kwa ugonjwa wa akili
- Maelezo kwa watu wanaosaidia kibinafsi
- Watu walioteuliwa: Jinsi ya kuteua na maana kwake.

### Brosha zingine zinapatikana kutoka:

- Baraza ya Afya ya Akili
- Huduma ya Utetesi wa Afya ya Akili
- Kituo cha Sheria ya Afya ya Akili.

Kwa maelezo zaidi kuhusu Sheria ya Afya ya Akili 2014 na nyenzo zingine, angalia tovuti ya Tume ya Afya ya Akili: www.mhc.wa.gov.au au pigia simu (08) 6272 1200.

This document can be made available in other languages and alternative formats on request.

Published by the Mental Health Commission (2015)

# Kupokea matibabu kwa ugonjwa wa akili



Brosha hii inakupa maelezo kuhusu haki zako ni nini na unachoweza kutazamia kama unapokea matibabu kwa ugonjwa wa akili.

## Matibabu ni nini?

Matibabu unayopokea kutoka huduma ya afya ya akili ni 'matibabu ya magonjwa wa akili' ambayo yanaweza kuwa pamoja na madawa, tiba ya mtukutiko wa umeme, matibabu yenye dharura ya magonjwa wa akili na utunzaji mwingine wa afya.

Ni haki yako kama mgonjwa kupokea matibabu mazuri sana yawezekanayo, na mtaalum wako wa magonjwa ya akili na wajumbe wengine wa timu wataongea nawe kuhusu uchaguzi wa matibabu. Utahusishwa na kupanga mpango wako wa matibabu, msaada na kuruhusu, na ruhusa yako (makubaliano) itatafutwa kila mara.

## Je, unaweza kutibwa kupinga nia yako?

Kama wewe ni mgonjwa wa hiari huwezi kupewa matibabu yoyote ya magonjwa wa akili bila ruhusa yako ya kujulishwa (au ruhusa iliyojulishwa ya mtu anayeweza kuamua maamuzi kwa ajili yako, kama mlezi). Ruhusa iliyojulishwa ina maana kuwa umepewa maelezo yote unayotaka na unayohitaji, na unaelewa kubisa uamuzi wako kukubali matibabu.

Kama matibabu ya magonjwa wa akili yanahitajika kuokoa maisha yako au kukuzuia kwa kusababisha madhara makali ya kimwili kwa wewe mwenyewe au mtu mwengine, yanaweza kukupewa bila ruhusa. Hayo yanaitwa matibabu yenye dharura ya magonjwa wa akili.

Kama wewe ni mgonjwa asiyekusudiwa (upo na agizo la matibabu ya mgonjwa aliyelazwa au agizo la matibabu ya jamii) unaweza kupewa matibabu ya magonjwa wa akili bila ruhusa yako, lakini bado uombewa kwa ruhusa yako.

## Unaweza kufanya nini kama huridhiki na matibabu yako?

Uanze na kuongea na timu yako ya tiba na kuzungumza uchaguzi wako ni nini.

Kama wewe ni mgonjwa wa hiari unaweza kuamua maamuzi yako kuhusu matibabu yapi unayokuwa tayari kukubali. Unaweza kuomba maoni ya pili kwa mtaalum mwengine wa magonjwa ya akili ukiwa kufanya hivi kutakusaidia kuamua unachotaka kufanya.

Kama wewe ni mgonjwa asiyekusudiwa unaweza kuomba yeyote mtaalum wako wa magonjwa ya akili au Mtaalum Mkuu wa magonjwa ya akili kupanga maoni ziada kwa wewe. Mtaalum wa magonjwa ya akili mwenye huru atakuchunguza na atatoa maoni yake kwa maandishi. Mtaalum wako wa magonjwa ya akili azingatie maoni hayo, lakini halazimishwa kufuata maoni ya ziada.

Baada ya kupokea maoni ziada unaweza pia kuomba mtaalum wako wa magonjwa ya akili, au Mtaalum Mkuu wa magonjwa ya akili, kupanga maoni ya kuongeza, lakini ombi linaweza kukataliwa.

Ukiwa bado hujaridhishwa, unaweza kumwombea Mtaalum Mkuu wa magonjwa ya akili kufikiria kesi yako. Mtaalum Mkuu wa magonjwa ya akili anaweza kumwomba mtaalum wako wa magonjwa ya akili kufikiria tena uamuzi kuhusu matibabu au anaweza kuacha.

## Matibabu ya uganga (kwa afya yako ya kimwili)

Wakati wewe ni mgonjwa, unaweza kutoa ruhusa kwa matibabu yoyote ya uganga unayoweza kuhitaji. Ukiwa huwezi kutoa ruhusa, mtu anayeruhusiwa kuamua maamuzi kwa ajili yako, anaweza kuruhusu kwa wewe. Kama wewe ni mgonjwa asiyekusudiwa hospitalini na unahitaji matibabu muhimu ya uganga, daktari yako hahitaji kupata kibali kukupa matibabu hayo, hata hivyo yeye amjulishe Mtaalum Mkuu wa magonjwa ya akili baadaye.

Kama wewe ni mgonjwa asiyekusudiwa hospitalini, unaweza kupewa ruhusa kwenda hospitali nyingine na kupata matibabu pale. Wakati upo na ruhusa bado wewe ni mgonjwa asiyekusudiwa ya kulazwa na uendelee kufuata mpango wako wa matibabu na kurudi ruhusa inapomalizia.

## Tiba ya mtukutiko wa umeme (ECT)

ECT ni matibabu kwa namba ya magonjwa ya akili. Ukiwa dawa yako haijaboresha hali yako, au kama ugonjwa wako ni mkali sana, mtaalum